OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI
LUPIRO,
S.L.P 288,
MAHENGE/ULANGA.

Mobile:0786617866
Kumb. Na LSS/A LEVEL/JOINING IN./2022/3
Mzazi/Mlezi wa:…………………………………………………………………………….
S.L.P …………………………………………………………………………………………….
Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 kwa tahasusi ya PCB – hongera sana. SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 08/09/2022
Shule ya sekondari Lupiro inapatikana mkoani Morogoro Wilaya ya Ulanga kata ya Lupiro 2km toka stendi ya mabasi ya Lupiro, barabara ya kuelekea Malinyi. Usafiri toka Morogoro na Dar es salaam upo kwa kupanda mabasi yanayoelekea Mahenge au Malinyi. Ukipanda mabasi yanayoelekea Malinyi utashuka kwenye kibao cha shule na ukipanda mabasi yanayoelekea Mahenge utashuka Lupiro mjini kisha utapanda pikipiki kwa gharama ya Tsh 1000/= tu.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1. sare ya shule

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote wa Masomo, anapokwenda Hospitali au anapokuwa kwenye shughuli zozote za kishule na nje ya eneo la shule. Aidha lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na mwanafunzi anapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo.

a. Shati nyeupe mbili za mikono mirefu(Tomato) kwa wote wavulana na wasichana Nembo ya shule inapatikana hapa shuleni.

b. Sketi mbili za rangi Light Blue(Cotton). Mshono wa sketi ni “Rinda box” iwe na rinda 1 kubwa mbele na rinda 1 kubwa nyuma, marinda 2 kushoto na marinda 2 kulia. Urefu wa sketi ni mpaka chini kwenye kifundo cha miguu kwa wasichana.

c. Suruali mbili za Light Blue zenye upana wa sm 16 – sm 20 chini zenye turn up kwa wavulana zinazogusa soli ya viatu.( USISHONE SURUALI ZA MODO)

   ( Ili kuepuka kuchanganya rangi ya vitambaa tunashauri mwanafunzi aje kushonea sare huku Lupiro)

d. Tai moja light Blue zenye zebra kwa wote wasichana na wavulana.

Edit with WPS Office

( Zinapatikana shuleni)

e. Soksi jozi mbili kwa wavulana za rangi ya kijivu na wasichana rangi nyeupe.

f. Sweta moja au zaidi rangi ya dark blue liwe la Mkenya na lisiwe la kufuma kwa ajili ya kuvaa wakati wa baridi.

g. T – shirt mbili (02) za sare ya shule kwa ajili kushindia baada ya masomo rangi ya dark blue na yenye kola (form six). (zinapatikana shuleni)

h. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kamba na vyenye kisigino kifupi. Usije na viatu visivyo na kamba.

i. Mikanda jozi mbili nyeusi yenye chuma shikizi (buckle ya heshima) kisicho kikubwa na isiyo na chata/alama yoyote.

j. Hijabu na nusu kanzu kwa wasichana wa kiislamu watakaopenda kuvaa hivyo wawe na suruali 2 za Light Blue (Cotton) upana sm 16 – sm 20 chini isiwe na turn up zinagusa soli,

2.2. VAZI LA KAZI.

-Wavulana suruali 2 nyeusi za kitambaa zenye turn up.

- wasichana magauni 2 rangi ya kijivu yenye kola mshono wa solo ya kumwaga, yenye marinda na mikono mifupi.

Wasichana wanaruhusiwa kuwa na suruali ya rangi ya light blue pana kwa ajili ya kusomea usiku (upana usizidi sm 24) Urefu iguse soli ya kiatu

2.3. SARE YA MICHEZO.

i. Truck suit 1 yenye rangi ya Light Blue yenye michirizi ya rangi ya nyeupe pembeni mikononi na miguuni

ii. T – shirt, bukta na soksi pair moja au zaidi zenye rangi ya Nyekundu yenye michirizi meupe ( Top – down - i.e, T – shirt nyekundu yenye michirizi ya meupe, bukta nyekundu yenye michirizi meupe na soksi nyekundu yenye michirizi meupe).

iii. Raba za kamba za aina ya michezo utakayo shiriki.

iv. Suruali ya jeje light blue

2.4. SARE YA SHULE ISIVALIWE NA VITU VIFUATAVYO:-

i. Kofia

ii. Herein, Bangiri, Pete, Mikufu.

Edit with WPS Office

iii. Viatu vya ghorofa.

iv. Vibanio vya nywele

v. Saa zenye urembo urembo (Iwe na mkanda wa kawaida wa chuma, ngozi au plastiki).

NB: Kamwe mwanafunzi asije na nguo zisizoelekezwa.

## 3. ADA NA MICHANGO YA SHULE.

### 3.1. ADA YA SHULE.

Ada ya shule kwa mwaka ni 70,000/= unaweza kulipa kiasi cha Tsh 35,000/= kwa muhula. Fedha hizo zilipe kwenye Account ya shule No. 21906600083 katika Benki ya NMB, jina la akaunti ni LUPIRO SECONDARY SCHOOL (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

### 3.2. MICHANGO MINGINE.

i. Tshs: 15,000/= Ukarabati na Samani kwa mwaka.

ii. Tshs: 6,000/= Kitambulisho na picha.

iii. Tshs: 30,000/= Kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.

iv. Tshs: 2,000/= kwa ajili ya Nembo.

v. Tshs: 10,000/= Huduma ya kwanza

vi. Tshs: 5,000/= Kwa ajili ya Tahadhari (haitarejeshwa).

vii. Tshs: 20,000/= kwa ajili ya Taaluma.

viii. Tshs: 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima.

NB

Kama una bima njoo nayo shule. Kwa wasio na bima mtafungulia huku kwa Tshs 5000 fedha za bima ya afya zisiwekwe kwenye akaunti ya shule

Kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonesha aina ya malipo watakayolipiwa na yatalipwa lini.

### 3.3. VFAA VYA MALAZI, CHAKULA NA USAFI:-

Edit with WPS Office

I. Jembe moja lenye mpini pamoja na kwanja moja.

II. Mifagio 02 mmoja kwa ajili ya kufagilia nje (chelewa zenye mpini) na mwingine kwa ajili ya kufagilia ndani (soft broom), squeezer na mopper

III. Godoro la $2^{1}/_{2}$ x 6

IV. Sahani, kikombe, kibakuli vya udongo na kijiko kwa ajili ya chakula Ndoo moja kubwa Lita 20 na moja ndogo Lita 10 za plastiki zenye mifuniko.

V. Chandarua kimoja chenye rangi nyeupe chenye pembe 4.

VI. Mashuka pair 2 kwa wasichana yenye rangi ya pink na pair 2 kwa wavulana yenye rangi ya light blue.

VII. Sandals pair 2.

VIII. Sanduku (Trunker).1

IX. Kanga pair 2 kwa wasichana na taulo 1 kwa wavulana.

X. Kandambili jozi aina ya umoja nyekundu.

XI. Sabuni za kuogea na kufulia.

XII. Dawa ya meno.

XIII. Mafuta ya kupakaa.

3.4. VIFAA VYA MASOMO:-

i. Madaftari zaidi 20 makubwa (Counter Book 3 Quire).

ii. Ream 2 za karatasi (A4 kwa mwaka).

iii. Kalamu ya wino wa bluu au nyeusi.

iv. Vitabu mbalimbali kulingana na masomo utakayosoma.

v. Dissecting kit wanaosoma Biology.

vi. Scientific Calculator isiyo programmable eg. FX 991 MS.

vii. Mathematical set 1.

NB: Simu za mkononi haziruhusiwi kabisa hapa shuleni Mwanafunzi haruhusiwi kuja na Simu adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule itachukuliwa kwa atakaepatikana na Simu.

4. FEDHA ZA MATUMIZI KWA MWANAFUNZI.

Mzazi/Mlezi unashauriwa umpe fedha za kutosha kwa matumizi yake, kuna duka la shule ambalo uwauzia wanafunzi mahitaji yao. Aidha haruhusiwi kuweka fedha nyingi

Edit with WPS Office

bwenini mwanafunzi aweke fedha kwenye akaunti yake ya benki.

## 5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

### A. HESHIMA

1. Mwanafunzi asimame na kumsalimia Mwalimu au mtu yoyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano.
2. Mwanafunzi hurusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yake na mwenzake, kwa mwalimu wake na kwa watu wengine.
3. Mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walio shuleni kama walezi wake.
4. Mwanafunzi ashirikiane na kusaidiana na wenzake katika kazi.
5. Mwanafunzi athamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
    a) Kuvuta sigara.
    b) Kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu wakati wote.
    c) Kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
    d) Kufuga ndevu.
    e) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
    f) Kugombana.
    g) Kusuka nywele.
7. Mwanafunzi aitike mara moja na kukimbilia aliko Mkubwa anayemwita.
8. Mwanafunzi aheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa wakuu wa Serikali, Nembo ya Taifa (Coat of Arms), Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Mwanafunzi aheshimu na kutunza ukumbi wa mikutano, mahali pa kuliachakula, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
10. Mwanafunzi anatakiwa kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Mwanafunzi awe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote alipo.
12. Mwanafunzi anyooshe mkono juu na kusimama anapoulizwa na kujibu maswali.
13. Mwanafunzi akae kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

Edit with WPS Office

## B. MAHUDHURIO.

1. Mwanafunzi ahudhurie shule kwa muda wote wa masomo.
2. Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na kuhudhuria maandalio ya masomo (preparation).
3. Mwanafunzi ahudhurie katika kazi zote za mikono.
4. Mwanafunzi ahudhurie mikusanyiko ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano mingine.
5. Kila mwanafunzi atapaswa kuhudhuria vipindi vya dini kikamilifu bila kukosa.
6. Mwanafunzi anaposhindwa kuhudhuria masomo au shughuli nyingine ya kishule kwa sababu ya UGONJWA lazima atoe taarifa kwa mwalimu wa zamu ili ampatie kibali kwenda kutibiwa na lazima aoneshe cheti cha mganga kwa mwalimu wa zamu baada ya kutibiwa.

## C. KUWAHI.

1. Kuwahi kuripoti mara shule inapofunguliwa.
2. Mwanafunzi awahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Mwanafunzi atii mlio wa kengele na kuwahi anapohitajika.

## D. MAWASILIANO

Mwanafunzi anapaswa kutumia lugha ya kiingereza wakati wote awapo shuleni.

## E. SARE ZA SHULE

1. Kila mwanafunzi atavaa sare ya shule:-
   a) Wakati wote wa masomo ya darasani.
   b) Wakati wote wa mihadhara ya shule (Baraza).
   c) Wakati wa kwenda hospitalini, mjini au maandamano. Rasmi.
   d) Wakati wote anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa vitu vifuatavyo pamoja na sare ya shule:-
   a) Viatu vya ghorofa.

Edit with WPS Office

b) Kofia isipokua waislamu wakati wa kwenda msikitini kuswali.

c) Mapambo mengine yoyote kama bangili, pete, mkufu, hereni, kupaka wanja, rangi ya mdomo na ya kucha.

d) Saa zenye urembo

3. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa viatu vya wazi jikoni.

## F. MIPAKA YA SHULE.

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum.

2. Mwanafunzi atatembelea sehemu zifuatazo kwa kibali maalum.

   a) Jikoni

   b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

3. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

   a) Vilabu vya pombe.

   b) Majumba ya starehe.

   c) Majumba ya kufikia wageni.

## G. USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi na ni sehemu ya maisha yake ya kila siku. Kwakhiyo kila mwanafunzi atazingatia yafuatayo:-

a) Usafi wa mwili wake na nguo zake.

b) Usafi wa ukumbi wa chakula.

c) Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

d) Usafi wa vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara.

Edit with WPS Office

e) Awe na nywele fupi – njiti ya kiberiti ikichomwekwa kwenye nywele ionekane. Haruhusiwi kusukwa nywele.

## H. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE BILA ONYO:-

1. Wizi wa vitu na wizi wa kalamu (forgery).
2. Uasherati, ubakaji na uhusiano wa jinsia moja.
3. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
4. Uvutaji wa sigara na bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa na Nembo zingine za Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani.ya shule
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kulala nje ya bweni bila ruhusa na kutoroka bwenini.
15. Kumiliki silaha ya aina yoyote.
16. Kumiliki kipasha joto(heater), pasi ya umeme, Radio, TV, Camera.
17. Kumiliki kukutwa na kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na kifaa chochote kinacho husiana na simu.
18. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
19. Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wezako, Walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
20. Kusuka nywele, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
21. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi.
22. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (Guest House).

Edit with WPS Office

23. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua, au kutishia.

## 6. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU.

Pamoja na barua hii pokea:

A. Fomu Namba B ya kupimwa afya yake. Apimwe kwenye hospitali ya serikali, hakikisha anapimwa siyo kujaziwa fomu tu. Na umweleze mganga matatizo ya afya aliyonayo. Kwani hatutapokea hoja zozote kinyume na ripoti ya daktari.

B. Fomu Namba C ya kuonyesha ndugu wa karibu na ahadi ya utekelezaji wa wajibu.

C. Fomu Namba D ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

D. Uje na nakala za cheti cha kuzaliwa/Affidavit Certificate, Leaving Certificate na result slip.

E. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi walioorodheshwa kwenye Fomu Namba C.

NB: Uje na faili ndani ukiweka fomu Na. B, C, D na viambatanisho vilivyotajwa kwenye D na E hapo juu.

❖ Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA SAFARI NJEMA KUJA KUJIUNGA NASI.
KAULI MBIU (MOTTO WA SHULE) NI: "ELIMU NI UKOMBOZI".

KARIBU SANA LUPIRO SEKONDARI

______________________

ANNETH M.CHENGULA
MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

PRESIDENT`S OFFECE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

SHULE YA SEKONDARI LUPIRO,

S.L.P 288,

MAHENGE/ULANGA.

_______________

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine ______________________ as to his/her physical and mental fitness for admission as a form FIVE at Lupiro Secondary School for the Academic year 2020/2021. Yours Sincerely.

……………………………….

ANNETH M. CHENGULA

THE HEADMISTRESS

The Headmaster, I have examine ____________________ at shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full – time Secondary School education.

1. Vision with/without glasses. Right ______________________________

   Left ______________________________

2. Blood pressure ______________________________

   Humoring ______________________________

3. Hearing ______________________________

4. (a) Urine Albumen ______________________________

   (b) Sugar ______________________________

5. (a) Venereal disease ______________________________

Edit with WPS Office

(b) Bilharzias ______________________________

6. Pregnancy ______________________________

7. Neurosis ______________________________

8. Is there any abnormality of:-
   (a) The heart ______________ (b) Lungs ______________
   (c) The spleen ______________________________
9. Are there any serious e.g. leprosy, diabetes, etc

   ______________________________

   Date ______________________ ______________________

   Station ______________________

Signature of medical officer______________________

Designation ______________________

**KIAMBATISHO "C" Ndugu wa karibu:** Hakikisha unaandika majina na anwani zao. Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo linatokea. Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a) Jina ………………………………… (b) Uhusiano ……………………………
   (c) Anuani …………………………………………………………………………
   (d) Kata ……………………………… (e) Mtaa ………………………………….
   (f) Namba ya ……………………………. (g) Balozi ………………………………..

2. (a) Jina ………………………………… (b) Uhusiano ……………………………
   (c) Anuani …………………………………………………………………………
   (d) Kata ……………………………… (e) Mtaa ………………………………….
   (f) Namba ya ……………………………. (g) Balozi ………………………………..

3. (a) Jina ………………………………… (b) Uhusiano ……………………………
   (c) Anuani …………………………………………………………………………
   (d) Kata ……………………………… (e) Mtaa ………………………………….
   (f) Namba ya ……………………………. (g) Balozi ………………………………..

4. (a) Jina ………………………………… (b) Uhusiano ……………………………
   (c) Anuani …………………………………………………………………………
   (d) Kata ……………………………… (e) Mtaa ………………………………….
   (f) Namba ya ……………………………. (g) Balozi ………………………………..

Sahihi ya mzazi ……………………………………….
Tarehe ………………………………………………….

Edit with WPS Office

AHADI YA KUTELEKEZA WAJIBU

Mimi …………………………………………………… nakubali nafsi niliyopata katika Shule ya Sekondari ya Lupiro kuendelea na masomo.
Nafahamu kuwa nimegharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi.
Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema.
Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.
Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu/malezi pamoja na wanafunzi wezangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule yangu na Taifa kwa ujumla.

…………………………………….

Sahihi ya mwanafunzi

Mimi …………………………………………mzazi/mlezi wa …………………………………..
Nimesoma maelezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anuani hiyo hapo chini:-
S.L.P ……………………………………………..
……………………………………………………
……………………………………………………
Jina la mzazi ………………………………………… Namba ya simu …………………………
Mtaa ………………………………………………….. Balozi …………………………………

## KIAMBATANISHO "D"

## FOMU YA MKATABA

A. KATI YA MWANAFUNZI NA SHULE.

1. Jina kamili kama alivyoandikishwa kwenye mtihani …………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………..
3. Mahali alipozaliwa ……………………………………………………………………
4. Dini ……………………………………………………………………………………
5. Shule alipomaliza elimu ya msingi …………………………. Wilaya ………………….

   Mkoa ………………………………. Mwaka aliomaliza ………………………………..
6. Shule alipomaliza elimu ya sekondari (kidato cha nne) ………………………………..

   Wilaya ………………………... Mkoa …………………………. Mwaka……………..

Mimi ……………………………………. Ninaahidi kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai kama yaliyoainishwa katika sheria za shule na nchi kwa ujumla.

Sahihi ………………………………………………… Tarehe ……………………………………..

Edit with WPS Office

B. KATI YA MZAZI NA SHULE.

Mimi …………………………………… Mzazi/Mlezi wa ………………………………………..

Ninakiri na kukubaliana na sheria za shule kama ambavyo zimeainishwa kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na makosa mengine ya jinai.

Aidha, nitakubaliana na hatua za kisheria atakazochukuliwa mwanangu ………………………….. endapo atakiuka taratibu za shule.

Sahihi …………………………………………………. Tarehe ……………………………………..



RANGI YA KITAMBAA CHA SKETI NA SURUALI

Edit with WPS Office